JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

---

**OFISI YA RAIS**

IKULU,
S.L.P 9120,
DAR-ES-SALAAM.

Kumb. Na. SHC/C.180/2/113

26 Juni, 2000

## WARAKA WA MKUU WA UTUMISHI WA UMMA NA. 1 WA MWAKA 2000

KUHUSU MAADILI YA WATUMISHI WA UMMA KATIKA MFUMO WA VYAMA VINGI VYA SIASA

## 1.0 UTANGULIZI:

1.1 Kuanzia mwaka 1965 hadi 1992 Tanzania ilipokuwa na Mfumo wa Siasa wa Chama Kimoja Watumishi wote wa Serikali na Vyombo vyake siyo tu waliruhusiwa bali ilionekana ni wajibu wao kushiriki katika mambo ya kisiasa. Shughuli nyingi za kiserikali na za kisiasa zilikwenda kwa pamoja na palikuwepo na maingiliano makubwa kati ya sehemu hizi mbili katika shughuli zote za kiutendaji, kiuongozi na kiitikadi.

1.2 Kufuatia mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliyofanyika Julai, 1992 na kuruhusu mfumo wa vyama vingi vya siasa, Serikali ilitoa maelekezo ya jinsi watumishi watakavyoshiriki katika mambo ya Siasa kupitia Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 1992.

## 2.0 UTARATIBU ULIOTOLEWA KATIKA WARAKA WA MKUU WA UTUMISHI WA UMMA NA.1 WA MWAKA 1992:

Utaratibu uliotolewa katika Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 1992 uliwagawa watumishi wa umma katika makundi mawili na kuweka Masharti ya namna watakavyoshiriki katika Siasa.

2.1 Watumishi wa Kundi "**A**" walijumuisha Watumishi wa ngazi za juu Serikalini, Serikali za Mitaa na katika Mashirika ya Umma wanaoshughulikia uandaaji na usimamizi wa sera. Hawa ni watumishi waandamizi wenye Madaraka kuanzia ngazi ya Mkurugenzi na kuendelea juu, Meneja Msaidizi na kuendelea juu na ngazi ya Mkurugenzi Mtendaji.

2.2 Watumishi wa Kundi "B" walijumuisha watumishi wa ngazi za chini na kati ambao hawahusiki na maandalizi ya sera mbalimbali.

2.3 Chini ya Waraka Na. 1 wa Mwaka 1992 watumishi katika Kundi "**A**" na "**B**" walipewa masharti kuhusu mambo wanayoruhusiwa na wasiyoruhusiwa kufanya.

## 3.0 KASORO ZILIZOJITOKEZA

3.1 Uzoefu ambao Serikali imeupata, kupitia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995 na pia uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika katika ngazi ya Mtaa, Kitongoji na Kijiji mwaka 1994 na 1999 umebainisha kuwa uhuru uliotolewa kwa watumishi wa umma kushiriki katika masuala ya siasa umeathiri Maadili ya msingi ya utendaji kazi Serikalini na vyombo vyake. Miongoni mwa athari hizo ni pamoja na tabia na vitendo vifuatavyo vya baadhi ya Watumishi wa Umma:

3.1.1 Kutotekeleza kwa dhati sera za Chama Tawala.

3.1.2 Kuikashifu Serikali kufuatana na msimamo wa kisiasa.

3.1.3 Kujihusisha na masuala ya siasa mahali pa kazi.

3.1.4 Kutoa huduma za kiutumishi kwa upendeleo unaotokana na msimamo wa kisiasa.

3.1.5 Kufanya shughuli za kisiasa wakati wa saa za kazi.

3.1.6 Watumishi wa Serikali Kuu kugombea nafasi za uongozi/ siasa katika Serikali za Mitaa jambo ambalo linakwenda kinyume na dhana ya kutenganisha Madaraka kati ya watungaji wa sera ambao ni viongozi wenye mwelekeo wa kisiasa na wale watekelezaji wa sera ambao kwa kawaida wanatakiwa kuwa watendaji.

3.2 Aidha, pamekuwepo utata kuhusu mgawanyo wa Watumishi katika makundi 'A' na 'B' kutokana na vigezo vyake kutoeleweka vizuri na hivyo wakati mwingine kusababisha mkanganyiko juu ya mtumishi yupi yuko katika kundi lipi.

3.3 Mbali ya makundi yaliyotajwa katika aya ya 2 hapa juu kuna makundi ya watumishi wa umma ambao hawakuorodheshwa katika Waraka huo lakini kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hawaruhusiwi kuwa wanachama wa chama chochote cha siasa wala kujihusisha na shughuli zozote za kisiasa isipokuwa kupiga kura tu. Watumishi hao ni:-

3.3.1 Askari wa Jeshi la Wanachi wa Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Polisi na Magereza (kwa mujibu wa Ibara ya 147(3) na (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

3.3.2 Majaji na Mahakimu wa ngazi zote (kwa mujibu wa Ibara ya 113A) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

3.3.3 Wajumbe na Watumishi wa Tume ya Uchaguzi na Wasimamizi wa Uchaguzi (kwa mujibu wa Ibara ya 74(14) na (15) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

3.4 Mbali ya makundi yaliyoorodheshwa katika Katiba kutoshiriki katika siasa yapo makundi mengine ambayo kwa mujibu wa kazi zao hayapaswi kushiriki katika siasa, lakini hayakutajwa katika Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.1 wa Mwaka 1992, mathalani, watumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa, Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Msajili wa Vyama vya Siasa, watumishi wa Ofisi ya Bunge, na Mawakili wa Serikali.

## 4.0 UAMUZI WA SERIKALI:

4.1 Kutokana na kasoro hizi zilizosababisha kumomonyoka kwa Maadili ya msingi ya Utumishi wa Umma Serikali imeamua kuhuisha Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.1 wa Mwaka 1992 kwa lengo la kudhibiti tabia na vitendo vinavyokiuka Maadili ya watumishi wa umma kwa kutumia kisingizio cha uhuru uliotolewa kushiriki katika mambo ya siasa.

4.2 Serikali imeamua kwamba hakutakuwa na makundi mawili ya watumishi kama ilivyokuwa hapo awali, bali watumishi wote wa umma sasa watatawaliwa na masharti yanayofanana.

4.3 Serikali pia imeamua kuainisha utaratibu utakaozingatiwa na watumishi wa umma watakaoamua kugombea ubunge kupitia viti maalumu, pamoja na wale watakaoteuliwa na Rais kwa mujibu wa Katiba kuwa Wabunge.

## 5.0 TAFSIRI YA MTUMISHI WA UMMA

Kwa madhumuni ya Waraka huu neno Mtumishi wa Umma lina maana iliyoainishwa katika Kanuni za Kudumu za utumishi wa umma toleo la 1994 kifungu Na.A.1(66). Nanukuu

*"Public officer or officers extends to and includes every person holding a public office invested with or performing duties of a public nature, whether under the immediate control of the President or not, and includes an officer under the control of a Local Government Authority or a Parastatal Organization, but does not include a person holding such an office only on part-time basis"*

## 6.0 UTARATIBU MPYA:

### 6.1 Madhumuni ya Utaratibu Mpya:

Madhumuni ya Waraka huu ni kuweka utaratibu mpya ambao pamoja na masharti yake, unazingatia umuhimu wa kuendelea kuwapa watumishi nafasi ya kutumia haki hii ya kikatiba kwa kuweka mipaka ili kuepuka madhara yanayoweza kuathiri utendaji wa shughuli za umma. Kwa hiyo lengo la Waraka huu ni kuonyesha mipaka na nafasi ya watumishi wa umma katika kushiriki katika mambo ya siasa na kuweka bayana mipaka ambayo haina budi kuzingatiwa kwa ukamilifu na kila mtumishi wa umma.

### 6.2 Maadili ya Msingi:

Watumishi wote wa umma wanapaswa kutambua na kuzingatia Maadili ya msingi ya utumishi wa umma yafuatayo:

6.2.1 Kutekeleza wajibu wao kama watumishi wa umma bila upendeleo wala ubaguzi kwa chama chochote cha Siasa ***(Political Neutrality/Impartiality).***

6.2.2 Kuwa na utii kwa Serikali ya chama kinachotawala ***(Loyalty)*** kwa kutekeleza kwa dhati na kwa ufanisi Sera za Serikali.

6.2.3 Kutoshiriki katika mambo ya siasa yanayozuia utendaji mzuri katika vyombo vya umma.

6.2.4 Kutoa huduma kwa misingi ya haki ***(fairness).***

6.2.5 Kufanya kazi kwa hekima na uadilifu ***(integrity).***

6.2.6 Kutunza siri za Serikali, Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma ***(confidentiality/secrecy).***

6.2.7 Kuheshimu maadili ya taaluma ***(professional ethics).***

## 6.3 Ushiriki wa Watumishi wa Umma katika Siasa:

6.3.1 Watumishi wa umma wanaruhusiwa kushiriki katika mambo ya siasa kama wakipenda. Hata hivyo, kwa kuwa hakuna **haki** isiyokuwa na **wajibu** wala **uhuru** usiokuwa na **mipaka,** watumishi wa Umma wanaruhusiwa kushiriki katika mambo ya siasa kwa utaratibu maalum ili kuhakikisha kwamba wanazingatia Maadili ya msingi yaliyoainishwa katika aya ya 5.2 hapa juu na kama yalivyofafanuliwa katika kijitabu cha ***Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma, Tanzania*** kilichotolewa na Idara Kuu ya Utumishi Serikalini, mwaka 1998.

### 6.3.2 Mambo Yanayoruhusiwa kwa Watumishi wa Umma:

Watumishi wote wa umma wanaoruhusiwa kushiriki katika mambo ya siasa wanaweza kushiriki katika shughuli zifuatazo: -

6.3.2.1 Kuanzia sasa hadi hapo itakapoamuliwa vinginevyo Mtumishi wa Umma anaruhusiwa kuwa mwanachama wa chama cha siasa anachokipenda, isipokuwa watumishi wale walioainishwa kwenye aya ya 8 ya Waraka huu.

6.3.2.2 Kupiga kura kwenye uchaguzi wa Rais, Wabunge na uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

6.3.2.3 Kuhudhuria mikutano halali ya kisiasa nje ya saa za kazi kama msikilizaji.

6.5.2.4 Kutoa michango yake binafsi kwa ajili ya chama chake akiwa nje ya mahali pa kazi na nje ya saa za kazi.

### 6.3.3 Mambo Yasiyoruhusiwa kwa Watumishi wa Umma:

Watumishi wote wa Umma wanaoruhusiwa kushiriki katika Siasa hawapaswi kushiriki katika shughuli zifuatazo:-

6.3.3.1 Kuajiriwa katika chama cha siasa wakati akiwa bado ni mtumishi wa umma

6.3.3.2 Kujishughulisha na shughuli za kisiasa wakati wa kazi na akiwa katika mahali pa kazi.

6.3.3.3 Kuvaa sare ya chama chochote cha siasa wakati wa kazi na mahali pa kazi.

6.3.3.4 Kutoa matamshi yanayoweza kuathiri hadhi ya Serikali kutokana na msimamo wake na imani yake ya kisiasa.

6.3.3.5 Kutoa huduma kwa ubaguzi kwa misingi ya imani ya kisiasa.

6.3.3.6 Kutoa siri za Serikali au Taasisi anayoitumikia.

6.3.3.7 Kutoa maoni katika mikutano ya hadhara ya kisiasa atakayohudhuria inayofanyika nje ya saa za kazi

6.3.3.8 Kugombea nafasi yoyote chini ya Katiba au uongozi wa ngazi yoyote katika chama cha siasa, akiwa mtumishi wa umma. .

6.3.3.9 Kumpigia kampeni mgombea yeyote wa nafasi ya uongozi chini ya Katiba au uongozi wowote katika chama cha siasa akiwa mtumishi wa umma.

6.3.4 **Utaratibu wa Kukoma Utumishi wa Umma:**

6.3.4.1 Iwapo Mtumishi wa umma ataamua:

(a) Kugombea nafasi yoyote chini ya Katiba, au

(b) Kugombea uongozi wa ngazi yoyote katika Chama cha Siasa,

Utumishi wa mtumishi huyo utahesabiwa kuwa umekoma tangu tarehe Tume ya Taifa ya Uchaguzi itakapo-mtangaza kuwa mgombea uchaguzi au tarehe yake ya kujiandikisha kugombea uongozi katika chama cha siasa au siku Tume ya Taifa ya Uchaguzi itakapomtangaza kuwa Mbunge/Diwani wa viti maalum.

6.3.4.2 Siku ya kukoma kwa mgombea uchaguzi anayetajwa katika aya 6.3.4.1(a) hapa juu ni siku Tume ya Uchaguzi inapotangaza majina ya wagombea (nomination day) au siku Tume ya Taifa ya Uchaguzi itakapomtangaza rasmi kuwa Diwani/ Mbunge wa viti maalum.

6.3.4.3 Siku ya kukoma utumishi wa Mtumishi anayetajwa katika aya ya 5.3.4.1(b) ni siku anayoamua kujiandikisha kuwa mgombea Uongozi wa chama kinachohusika.

6.3.4.4 Mtumishi ambaye utumishi wake umekoma chini ya utaratibu ulioainishwa katika aya ya 6.3.4.2 na 6.3.4.3 atalipwa stahili zake zote za utumishi kulingana na Sheria za mafao nchini.

6.3.4.5 Endapo mtumishi wa umma atashindwa katika Uchaguzi na akataka kurejea katika utumishi wa umma hana budi kuomba ajira upya kwa Mamlaka zinazohusika.

6.4 **Utaratibu wa Utumishi kwa Mtumishi wa Umma Anayeteuliwa na Rais kuwa Mbunge:**

6.4.1 Mtumishi wa umma anayeteuliwa na Rais kuwa Mbunge kwa mujibu wa Ibara ya 66(1)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyorekebishwa na Sheria Na.3 ya Mwaka 2000 atahiari kuchagua moja kati ya mambo yafuatayo:-

(a) Kuchukua likizo bila malipo hadi atakapomaliza kipindi chake cha uteuzi, au.

(b) Kujiuzulu katika utumishi wa umma na kulipwa mafao yake kulingana na sheria za mafao nchini.

6.4.2 Hata hivyo atakapomaliza likizo yake baada ya kipindi chake cha uteuzi, kurejea kwake kazini kutategemea kuwepo kwa nafasi ya kazi ya kuweza kumuajiri katika utumishi wa umma.

6.4.3 Iwapo mtumishi wa umma atasita kupokea uteuzi wa Rais ataruhusiwa kuendelea kuwa mtumishi wa umma.

6.5 **Watumishi wa Umma Waliokwishachaguliwa Uongozi wa Vyama na Serikali za Mitaa:**

Watumishi wa Umma waliokwishachaguliwa katika ngazi za uongozi wa vyama na Serikali za Mitaa kabla ya Waraka huu wanaruhusiwa kuendelea katika nafasi zao hadi vipindi vyao vya uongozi vitakapomalizika.

## 7.0 WAKATI WA KUJITAYARISHA/KUJIANDIKISHA KUWA MGOMBEA

Mtumishi atakayeamua kugombea atatakiwa kutoa taarifa rasmi kwa Mamlaka iliyomuajiri na kisha ataomba na atapewa likizo bila malipo ili akashughulikie taratibu zake za kugombea nafasi aliyoomba. Aidha, utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:-

7.1 Kwa Wagombea Ubunge wa Majimbo ya Uchaguzi na Madiwani Likizo hiyo itaanzia tangu siku ya kuvunjwa Bunge na itakoma tarehe ya kuteuliwa na Tume ya Uchaguzi kuwa mgombea (Nomination day).

7.2 Kwa upande wa viti maalum likizo hiyo itaanzia tangu siku ya kuvunjwa Bunge hadi tarehe Tume ya Uchaguzi itakapomtangaza kuwa Diwani au Mbunge.

## 8.0 WATUMISHI WA UMMA WASIORUHUSIWA KUSHIRIKI KATIKA SIASA:

8.1 Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania makundi ya Watumishi wasioruhusiwa kuwa Wanachama wa Chama chochote cha Siasa wala kujihusisha na shughuli za kisiasa isipokuwa kupiga kura ni kama ifuatavyo:-

8.1.1 Askari wote wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Polisi na Magereza (kwa mujibu wa Ibara ya 147(3) na (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

8.1.2. Majaji na Mahakimu wa ngazi zote (kwa mujibu wa Ibara ya 113A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

8.1.3 Wajumbe na Watumishi wote wa Tume ya Uchaguzi na Wasimamizi wa Uchaguzi (kwa mujibu wa Ibara ya 74(14) na (15) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

8.2 Vyombo vingine vya utendaji Serikalini ambavyo kwa hulka yake na kwa mujibu wa utendaji wake wa kazi Watumishi wake hawaruhusiwi kuwa Wanachama wa chama chochote cha siasa na kushiriki katika mambo ya Siasa ni pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Idara ya Usalama wa Taifa, Mawakili wa Serikali, na watumishi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

## 9.0 NIDHAMU:

9.1. Maadili haya yatakuwa sehemu ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ***(Standing Orders for the Public Service)*** na kanuni nyingine mbalimbali za Utumishi wa Umma ***(Service Regulations)*** ambazo zitarekebishwa ipasavyo.

9.2. Masuala ya nidhamu yanahitaji usimamizi wa karibu, hivyo kila Mtendaji Mkuu, Kiongozi wa Idara na Sehemu katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Taasisi nyingine za umma anaagizwa kuhakikisha kwamba Watumishi walio chini yake wanagawiwa Waraka huu na wanaelimishwa ipasavyo kuhusu masharti ya Waraka huu ili hatimaye wayazingatie kwa ukamilifu bila visingizio vya aina yoyote ile.

9.3. Aidha, ni muhimu kila Mtumishi wa Umma kujua na kuelewa nafasi, haki na wajibu wake katika utaratibu wa Mfumo wa Demokrasia ya vyama vingi vya siasa ili ushiriki wake katika siasa usiathiri vibaya ***HIARI*** yake ya kuwa mtumishi wa umma na utendaji wake wa kazi katika sehemu yake ya kazi.

9.4. Mtumishi wa umma atakayekiuka masharti ya waraka huu atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo katika chombo anachokitumikia. Aidha, anaweza kuchukuliwa hatua za kisheria kulingana na kosa atakalobainika kulitenda.

## 10.0 TAMATI

Waraka huu unatolewa chini ya Sheria ya Utumishi Serikalini Na. 16 ya mwaka 1989 Kifungu 4(1) na unaanza kutumika tarehe ***1 Julai, 2000.*** Aidha, Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 1992 unafutwa.

M.Y.C. LUMBANGA
*Katibu Mkuu Kiongozi na*
*Mkuu wa Utumishi wa Umma*

Imepigwa Chapa na Mpigachapa wa Serikali— Dar es Salaam, Tanzania

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

IKULU,
S.L.P. 9120,
DAR ES SALAAM.

KUMB. NA. SHC/C. 180/2/152 22 Aprili, 2002

## WARAKA WA MKUU WA UTUMISHI WA UMMA NA.1 WA MWAKA 2000

## REKEBISHO NA.1

### KUHUSU WAGOMBEA UDIWANI, WAGOMBEA UBUNGE WA VITI MAALUM, UBUNGE WA KUTEULIWA NA RAIS KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA WAGOMBEA UBUNGE KATIKA BUNGE LA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

1.0 Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.1 wa Mwaka 2000 uliweka Masharti yanayowaongoza Watumishi wa Umma kushiriki katika shughuli za Kisiasa nchini.

2.0 Baada ya Masharti hayo kutumika kwa muda wa takriban mwaka mmoja na nusu, Serikali imeamua kufanya marekebisho katika Waraka huo kwa lengo la kuboresha Masharti hayo kwa Watumishi wa Umma watakaoamua kugombea au watakaoteuliwa katika nafasi zilizotajwa hapo juu kama ifuatavyo:

2.1 **Watumishi wa Umma wanaoamua kugombea Udiwani**

Watumishi wa Umma watakaoamua kugombea Udiwani wanaruhusiwa kufanya hivyo na endapo watabahatika kushinda wataendelea na ajira zao kwani Udiwani sio ajira.

Hata hivyo Watumishi wa Umma ambao ni waajiriwa katika Halmashauri *(Council)* hawaruhusiwi kugombea Udiwani katika Halmashauri wanazofanyia kazi.

2.2 **Watumishi wa Umma Wanaoamua Kugombea Ubunge Kupitia Viti Maalum**

Watumishi wa Umma watakaoamua kugombea Ubunge kupitia Viti Maalum wanaruhusiwa kufanya hivyo na endapo watashinda wana hiari ya ama kuacha kazi na kulipwa mafao yao au kuchukua likizo bila malipo kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge tangu Tume ya Uchaguzi itakapowatangaza kuwa Wabunge.

2.3 **Watumishi wa Umma Wanaoteuliwa na Rais Kuwa Wabunge kwa Mujibu wa Ibara ya 66(1)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 *(Toleo la Mwaka 2000)***

Watumishi wa Umma watakaoteuliwa na Rais kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 66(1)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ***(Toleo la Mwaka 2000)*** wana hiari ya ama kuacha kazi na kulipwa mafao yao au kuchukua likizo bila malipo kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge kuanzia siku watakayoteuliwa.

2.4 **Watumishi wa Umma Watakaogombea Ubunge Katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki**

Watumishi wa Umma watakaochaguliwa kuwa Wabunge katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaweza kuendelea na kazi katika Utumishi wa Umma au kuchukua likizo bila malipo. Aidha, wakati wa kuhudhuria Vikao vya Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki watalazimika kutoa taarifa kwa Waajiri wao na watapewa ruhusa maalumu ya kuhudhuria Vikao hivyo.

3.0 MWISHO

Masharti mengine yanabaki kama yalivyo. Aidha, marekebisho haya yatatumika kuanzia tarehe ya Waraka huu; isipokuwa kwa Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki marekebisho haya yatatumika kuanzia tarehe 15 Juni, 2001.

M. Y. C. Lumbanga,
KATIBU MKUU KIONGOZI
NA
MKUU WA UTUMISHI WA UMMA

UMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA WA SERIKALI, DAR ES SALAAM — TANZANIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

IKULU,
S.L.P. 9120,
**DAR ES SALAAM**

Kumb.Na. CAB 157/539/01/42 16 Septemba, 2009

**WARAKA WA MKUU WA UTUMISHI WA UMMA NA.1 WA MWAKA 2000**

**REKEBISHO NA. 2**

**KUHUSU WATUMISHI WA UMMA KUGOMBEA NAFASI ZA UONGOZI KATIKA SERIKALI ZA MITAA**

1.0 Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2000 uliweka masharti yanayowaongoza Watumishi wa Umma kushiriki katika shughuli za kisiasa nchini.

2.0 Baada ya Masharti hayo kutumika kwa muda wa takriban mwaka mmoja na nusu yaani Aprili, 2002,. Serikali iliamua kufanya marekebisho katika Waraka huo kupitia **REKEBISHO NA. 1** kwa lengo la kuboresha Masharti hayo kwa Watumishi wa Umma watakaoamua kugombea au watakaoteuliwa katika nafasi za Udiwani, Ubunge wa Viti maalum,Ubunge wa Kuteuliwa na Rais katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wagombea Ubunge katika Bunge la Afrika Mashariki.

3.0 Waraka huo wa Mkuu wa Utumishi wa Umma sasa umetumika kwa takriban miaka tisa (9) na Serikali imeamua kuufanyia marekebisho kwa lengo la kuboresha masharti hayo, hususan kuhusu Watumishi wa Umma watakaopenda kugombea nafasi ya Mwenyekiti wa kijiji, Kitongoji au Mjumbe wa Halmashauri ya kijiji kwa upande wa Halmashauri za Wilaya au Mwenyekiti wa Mtaa au Mjumbe wa Kamati ya Mtaa kwa upande wa Halmashauri za Miji kama ifuatavyo:

3.1 Watumishi wa Umma ambao ni waajiriwa katika Halmashauri (Councils) hawaruhusiwi kugombea nafasi yoyote katika Kijiji, Kitongoji au Mtaa katika Halmashauri wanazofanyia kazi.

3.2 Masharti mengine kuhusu ushiriki wa Watumishi wa Umma katika shughuli za siasa yanabaki kama yalivyo.

**4.0 MWISHO.**

Marekebisho haya yatatumika kuanzia tarehe 16 Septemba, 2009.

(Phillemon L. Luhanjo)
**KATIBU MKUU KIONGOZI NA**
**MKUU WA UTUMISHI WA UMMA**